



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA
KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA



Unapojibu tafadhali taja:

29 Disemba, 2022

BC.143/234/02/61

Mkurugenzi
Halmashauri wa Wilaya ya Kaliua
S.L.P 83
Kaliua Tabora

**Yah: UTHIBITISHO WA UWEPO WA ARDHI KWA AJILI YA KAMPUNI YA YFH
INTERNATIONAL BUSINESS COMPANY LIMITED**

Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimepokea ombi la kampuni ya YFH INTERNATIONAL BUSINESS CO. LTD la kusajili mradi wa kilimo cha mazao ya chakula na biashara katika kijiji cha Limbula kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

2. Baada ya kupitia maombi yake pamoja na nyaraka alizoambatanisha, tumegundua kuwa ofisi yako imekuwa na mawasiliano ya kimaandishi na mwekezaji huyo kwa ajili ya kumsaidia kupata ardhi ya uwekezaji hicho.

3. Kwa kuzingatia ukubwa wa ardhi anayohitaji ya hekari 6000 na kwa kuwa ardhi hiyo ipo kwenye Halmashauri yako, Kituo kinaomba kupatiwa UTHIBITISHO kutoka ofisi yako ya uwepo wa ardhi tajwa na kama haina mgogoro wowote, pia mkataba wa mwekezaji na wauzaji kwa ajili ya kutekeleza mradi wa mwekezaji huyo. Uthibitisho huo utatusaidia kuendelea na mchakato wa kusajili mradi tajwa wakati taratibu za kuhaulisha ardhi husika zikianza kutoka katika ofisi yako.

4 Tunatanguliza shukrani za dhati kwa ushirikiano wako

A. Lyimo

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI